# SHULE YA UPILI KAPSABET  JARIBIO LA KWANZA 2025

## MWONGOZO WA KUSAHIHISHA

**SEHEMU YA A.: FASIHI SIMULIZI**

1. Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali yaliyoulizwa. (al. 20)

Kondolo, kondolo
Mlezi wa mwana
Mai kenda, nani kenda
Sokoni kenda
Kondolo, we ndolo mwana.

Mai tarudi atarudi
Adazi lako akirudi
Pia nyama ya kufupa
Kufupa kwangu wewe msopa
Kipenzi mwana

Kondolo kindolo
Mwana ndolo
Mwana kuja
Titi laja
Basi ndolo kipenzi cha mama
Ndolo ndolo atarudi.

a. Huu ni wimbo wa aina gani? Kwa nini? (al. 4)

**-Bembelezi**

**-Ni motto ambaye anaimbiwa**
**- Anaambiwa asulale titi laja**
**- Mlezi ametajwa**
**- Mama akirudi atamletea zawadi**

b. Tunga wimbo mfupi wa aina hii kutoka jamii yako. (al. 6)

**(Mwalimu atathmini jibu la mwanafunzi)**

c. Taja mbinu zozote mbili za lugha katika wimbo huu. (al. 6)

**Takriri- kondolo kondolo, ndolo ndolo**
**Jazanda – titi linasimamia mama**

d. Kuna wahusika wangapi katika wimbo huu? Wataje. (al. 2)

**Wawili – Mwimbaji**

- **Mlezi**

- **Kondolo - mtoto**

e. Eleza uhusiano wa wahusika uiliowataja katika swali la 4. (al.2)
**Huyu ni mlezi na mtoto**

2. **SEHEMU YA B. TAMTHILIA**

***T. Arege: Bembea Ya Maisha***

…Jamani mtoto amejaribu! hivi umesahau kuwa hata wewe unatumia hele za kununua dawa? Hata sasa umetumia mapeni uliyotumiwa wasikuone shabiki tu.

a.Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)
**Anayezungumza - Sara**
**Anayezungumziwa – Yona**
**Mahali – Nyumbani**
**Tukio – Wakati Yona na Sara walipokuwa wakizungumzia kuhusu mambo Neema alikuwa amewatendea**.

b. Tambua na ueleze mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo. (al.4)
**Balagha – Anakutumia hela za kununua dawa?**
**Nidaa – Jamami motto amejaribu!**

c. Onyesha jinsi mhusika anayerejerewa amejaribu kuwashika mkono wazazi wake. (al.4)
**Analipia malibabu**
**Kuajiri mgfanyakazi**
**Kuwanunulia jiko la gesi.**
**Kumpa Yona pesa**
**Kulipia wanuna wake karo**

d. Taja sifa nane za anayerejelewa. (al. 8)
**Mkarimu**
**Msomi**
**Amewajibika**
**Mwenye utu**
**Mwenye bidii**
**Mwenye busara**
**Mwenye upole**
**Mwenye heshima**

3. Jadili nafasi ya mwanamke katika jamii ya bembea ya Maisha. (al. 20)
**Mwerevu – Sara**
**Mwenye hekima – Sara**
**Kujifungua watoto wa kiume na kike – Sara**
**Wa kusutua – Sara**
**Mvumilivu – Sara/Welma**
**Mshauri mwema – Sara**
**Mwajibikaji – Neema/Sara/Dina**
**Wakunyimwa elimu – Sara**

**Kiumbe dhaifu – Sara**
**Mtamaduni – Sara**
**Msimamodhabiti – Sara/binti za Sara**

4. **SEHEMU YA C. RIWAYA**

**C. Momanyi:Nguu za Jadi**

Jadili maudhui yafuatayo yanavyo jitokeza katika Riwaya ya Nguu za Jadi.

i. Ufisadi (al. 10)

- **Watu kuajiriwa kwa msingi ya kujuana.**
- **Umesababisha mauaji ya kifamilia.**
- **Polisi wamamwangaisha Lonare kwa kuwatoza maderava wa Lonare faini zisizowlwweka.**
- **Sagila kumwohonga Mangwasha ili afaidi penzi lake.**
- **Sihaba analipwa na Sagila kusambasa vijikaratasi vya uchochezi.**
- **Mtemi Lisulia kuamuru jalada la ardhi ya matongo kufichwa.**
- **Mashtaka yaliyofikishwa koetini huzimwa kabla ya kesi kuanza.**
- **Taasisi ya magereza ni fisadi kuwafungulia wahalifu kama Silaba watoke.**
-

ii. Ukabila (al. 10)

**- Wakule ndio wengi serikalini.**
**- Kazi za madaraka ziliwaendea wakule**
**- Umesababisha ukosefu wa ajira – waketwa**
**- Majina ni kigezo cha kupimia ajira**
**- Mangwasha anadhurumiwa na chifu kwa sababu ya kabila lake.**
**- Chuki ya Mtemi Lesulia kwa Lonare inatokana na ukabila.**
**- Maneno ya hisia za ukabila kuhusu wakitwa.**

5. Taja na ueleze sifa za wahusika wafuatao .(al 20)

i. Sagilu

- **Mwenye ukabila**
- **Fisadi**
- **Mwenye tamaa**
- **Mwenye ubinafsi**
- **Katili**
- **Mnafiki**
- **Msaliti**

ii. Mangwasha

- **Mvumilivu**
- **Mzalendo**
- **Jasiri**
- **Mtiifu**
- **Aliyejikomboa kimawazo**
- **Mwajibikaji**

iii. Mtemi lesulia

- **Mwenye tamaa**
- **Mwenye ubinafsi**
- **Fisadi**
- **Mdanganyifu**
- **Katili**
- **Mnafiki**
- **Msaliti**

iv. Chifu Mshabaha

- **Mwenye ukabila**
- **Fisadi**
- **Katili**
- **Msaliti**
- **Mwenye dharau**

**6 SEHEMU D -USHAIRI**

a) Huru- kwa sababu hauzingatii kanuni (kutaja 1 maelezo1)

b) Kuonyesha jinsi mwanamke anavyoonewa kwa sababu ya jinsia yake.

c) Mishata ni mistari ya shairi ambayo haijakamilika m.f. Hujidadisi kuja kwa nini. Hukaa na kujiuliza.
(kutaja 1 mifano 2×½=2)

d) i) Balagha
ii) Takiriri- mfano wazia jidadisi wapi (2×2=4)

e) Nafsineni ni mwanamke .

f.) Toni ya huzuni/ majonzi/ kutamauka

g) <u>Maudhui.</u>
i) dhiki za ulezi
ii) kudhalilishwa kazini
iii) Kudhalilishwa kwa sababu ya jinsia (2×1=2)

h) Usaliti- wanawake wa nzake kutomuunga mkono. (1×2=2)
i) Madhila- matatizo/ shida
ii) Kudhalilishwa- Kudharauliwa/ kudunishwa/ kunyanyasa.

7.a) ukiukaji wa maadili ya kikazi

i. majaji wanaostahili kutetea haki ni walaji rushwa
ii. madaktari hawawajibiki kwa matibabu na kuwa’ magonjwa hayatibiki
iii. madaktari wanakwerida kinyume na kiapo chao kwa kuweka pesa mbele.
iv. Licha ya mbwembwe nyingi za kiapo cha mawaziri, wana mikataba ghushi.
v. Magavana wanatafuna nchi na kuwa haikaliki.
vi. Viongozi ni wanafiki hawaaminiki.
vii. Maraisi wanashabikia wizi.
viii. Waapaji ni wanafiki **Zozote 3 x 1 =3**

b) i) usambamba

i. Kila ubeti unaanza kwa neno kiapo

ii. Sehemu ya utao ya mshororo wa tatu katika kila ubeti inarudiwa katika kimalizio

**alama 2 x 1 =2**

ii

i. Taswira oni— kiapo cha mawaziri, shingo tai haitoki
ii. Taswira sikivu- kwa mizinga na fataki
**iii.** Taswira mwonjo- wengi wao ni walaji a**lama 3 x 1 = 3**

c) toni katika shairi

i. Kulalamika- kuna ukosefu wa uwajibikaji kazini
ii. Kushtumu/ kusuta- majaji wanaostahili kutetea haki ni walajirushwa 1×2=2

d) idhini/ uhuru wa mshairi

i. Utohozi- feki
ii. Kuboronga sarufi- shingo tai haitoki
iii. Inkisari- wanosimama- wanaosimama a**lama 2x2=4**

e)

i. Mpangilio wa vina- ukara- vina vya nje vinatiririka ilhali vya ndani vinabadilika badilika
ii. Mizani- msuko- kimalizio kimefupishwa
iii. Mpangilio wa maneno- kikwamba- neno kiapo limetumika kuanzia mwanzo wa kila ubeti.
Pindu- sehemu ya utao ya mshororo wa tatu katika kila ubeti inarudiwa katika kimalizio

**3x1=3**

f) i) shairi hili lina beti tano
ii) kila ubeti una mishororo minne
iii) lina pande mbili; ukwapi na utao
iv) kituo kimefupishwa
v) vina vya nje vinatiririka ilhali vya ndani havitiririki
vi) mizani 16 kwa kila mshororo ila kwa kituo ni nane. **Zozote 3x1=3**